


# Kuku na Tai



Ann Nduku ✎  
Wiehan de Jager ✎  
Matteo E. Mwita 📄  
3  
Kiswahili! 🗨️ MS



# Global Storybooks

[globalstorybooks.net](http://globalstorybooks.net)


## Kuku na Tai

Ann Nduku ✎  
Wiehan de Jager ✎  
Matteo E. Mwita 📄




This work is licensed under a Creative Commons Attribution 3.0 International License.  
<https://creativecommons.org/licenses/by/3.0>







Hapo zamani za kale, Kuku na Tai walikuwa marafiki. Waliishi kwa amani na ndege wengine. Hakuna kati yao aliyeweza kupaa.




Kila kivuli cha mabawa ya Tai kinapoonekana ardhini, Kuku huwatahadharisha vifaranga vyake. "Tokeni kwenye eneo la wazi." Na wanajibu: "Sisi si wajinga. Tutakimbia."




Kuna siku njaa ilitokea. Ikamlazimu  
Tai kutembea umbali mrefu  
kutafuta chakula. Alirudi akiwa  
amechoka sana. "Lazima kuwe na  
njia rahisi ya kusafiriri!" Tai alisema.




Tai aliporudi siku iliyofuata,  
alimkuta kuku akichakura  
mchangani, ila hakukuwa na  
sindano. Kwa hiyo Tai alishuka kwa  
kasi na kukwapua kifaranga kimoja.  
Akaondoka nacho. Tangu hapo, kila  
Tai anapojitokeza humkuta kuku  
akichakura kwenye mchanga  
akitafuta sindano.




Baada ya usingizi mnono wa usiku, Kuku alijiwa na wazo zuri sana. Akaanza kukusanya manyoya yaliyodondoka kutoka kwa ndege wenzao. "Tuyashonee haya manyoya juu ya manyoya yetu," Kuku alisema. "Labda itaturahisishia kusafiri."




"Nipatie siku moja," Kuku alimwomba Tai. "Halafu utaweza kushona bawa lako na kuruka tena kwenda kutafuta chakula." "Siku moja tu," alisema Tai. "Kama hutaipata sindano, itabidi unipe kimoja cha vifaranga vyako kama malipo."




Tai pekee ndiye aliyekuwa na  
sindano kijijini, kwa hiyo akaanza  
kushona wa kwanza.  
Akajitengenezea mabawa mawili  
mazuri na akapaa juu ya kuku. Kuku  
aliazima sindano lakini akachoka  
kushona baada ya muda mfupi.  
Akaacha sindano kabatini na  
akaenda jikoni kuandaa chakula kwa  
ajili ya watoto wake.



Baadaye jioni Tai akarudi. Akamba  
sindano ili aweze kushona baadhi ya  
manyoya yaliyokuwa yameanza  
kulega alipokuwa safarini.  
Akaangalia kwenye kabati.  
Akaangalia jikoni. Akaangalia uani.  
Ila sindano haikupatikana.



Lakini ndege wengine walimwona Tai akipaa. Wakamwomba Kuku awaazime sindano ili nao wajishonee mabawa pia. Muda si mrefu ndege wakawa wamepaa na kuzagaa anga zima.



Ndege wa mwisho aliporudisha sindano aliyoazima, Kuku hakuwepo. Kwa hiyo watoto wake wakachukua sindano na wakaanza kuichezea. Walipochoka na mchezo wao, wakaiacha sindano kwenye mchanga.